JESMA 002

# TATHMINI YA AWAMU AWALIA
## GREDI YA SABA 2024
## - KISWAHILI -

002-2024

**Muda: Saa 1 dakika 30**

Jina la mwanafunzi: .................................................... Nambari ya Tathmini: ............................

Shule: ........................................................................ Gredi 7:................ Tarehe: ..............................

**(Alama 40)**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 1 hadi la* **5**

***(Ni katika mji mmoja kijana Tonui anatembea barabarani polepole. Anaonekana akiwa na wasiwasi. Wanakutana na Mzee anayeonekana mchafu kiasi )***

| | |
|---|---|
| Mzee wa kwanza: | Habari yako kijana? |
| Tonui: | Nzuri sana. |
| Mzee wa kwanza: | Samahani kijana wangu. Mimi nimetoka mashambani. Siujui mji. Je, unaweza kunieleza ziliko ofisi za wazimamoto ziko wapi? |
| Tonui: | Ninasikitika hata mimi siujui mji. Nimefika asubuhi kutoka mashambani. Nilikuwa nimekuja kumtembelea mjomba wangu ili anipe pesa za kulipia ziara ya kutembelea mbuga ya wanyamapori wiki ijayo. |
| Mzee wa kwanza: | Mjomba wako anafanya kazi wapi? |
| Tonui | Yeye ni mwalimu katika shule moja hapa mjini. |
| Mzee wa kwanza: | Je, mjomba wako amekusaidia? |
| Tonui: | Ndio, amenisaidia. Amenipa pesa za kulipia safari hiyo na nyingine nipelekee mama za matumizi ya nyumbani. |
| Mzee wa kwanza: | Sasa unaelekea wapi? |
| Tonui: | Ninataka kujionea mji kidogo halafu niabiri gari kuelekea mashambani. |
| Mzee wa kwanza: | Kama ni hivyo basi nisaidie kutafuta ofisi za wazimamoto |
| Tonui: | Unamtafuta nani huko? |
| Mzee wa kwanza: | Kaka yangu hufanya kazi huko. Yeye ni dereva wa lori. Mke wake ni mgonjwa ndiye amenituma nije nichukue pesa za kwenda hospitalini. |
| Tonui: | Pole. Basi ni vyema umtafute akupatie hela hizo. |
| Mzee wa kwanza: | Ndiyo sababu ninakuomba unisaidie. *(analengalengwa na machozi)* |
| Tonui: | Basi tujaribu kuitafuta. *(Mzee anamwongoza na wanaondoka)* |
| Mzee wa kwanza: | (*Anamsimamisha mpitanjia*) Tafadhali ndugu tueleze ziliko ofisi za wazimamoto. |
| Mpitanjia: | Fuateni njia hii. Mkifika upande ule mwingine mtaona ofisi hizo. *(Wanafuata kichochoro huku wakiongea). (Mtu mmoja anatoa karatasi mfukoni na kuiangusha)* |
| Mzee wa pili: | Simameni hapo hapo. Mimi ni askari wa mji. **Ninawatia mbaroni** kwa kuchafua mji. |
| Mzee wa kwanza: | Tafadhali askari tuonee huruma. |
| Mzee wa pili: | La! Nitawapeleka korokoroni. Siku ya mtondo kutoka leo, mtapelekwa kortini kujibu mashtaka ya kuchafua mji. |
| Mzee wa kwanza: | (*Akitokwa na machozi*). Tafadhali tusamehe. Hatutarudia tena. Tuko tayari kukupa kitu kidogo.. |
| Mzee wa pili: | Mzee, nitakushtaki pia kwa kujaribu kunipa hongo. |
| Tonui: | (*Anaanza kulia*)Tafadhali tusamehe. |
| Mzee wa pili: | Kama ni hivyo, toeni pesa zote mlizo nazo. |
| Mzee wa kwanza: | (*Anatoa noti kadhaa*). Mimi nina hizi pekee. Kijana wangu, tafadhali toa zile ulizo nazo ili tusipelekwe korokoroni. |
| Tonui: | (*Anatoa pochi*) Mimi nina hizi pekee. |
| | (*Mzee wa pili anachukua pochi na kuwaambia waondoke*) |
| | (*Mzee wa kwanza anatimua mbio. Tonui anaondoka polepole akilia*) |

1. Mazungumzo haya yamehusisha watu wangapi? ____________ (al 1)

2. Unafikiri mzee wa kwanza alikuwa ametumwa kutoka mashambani?

____________ (al 1)

3. Ikiwa leo ni Jumanne, je, mtondo itakuwa siku gani? ____________ (al 1)

4. Msemo '**kutiwa mbaroni**' ni ____________ (al 1)

5. Kwa mujibu wa mazungumzo uliyoyasoma, unafikiri Mzee wa kwanza na wa pili walifanya nini baadaye? (al 1)

____________

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la* **6** *hadi la* **10**

Umuhimu wa muziki hasa huwa ni nini? Watunzi wa nyimbo mbalimbali huwa wana msukumo upi? Lengo lao huwa lipi? Ni mambo yapi hutazamwa kabla ya wimbo fulani kupigiwa debe kuwa ni mzuri?

Najua vyema kuwa ni muhali binadamu wote katika mazingira yoyote yale kuungana kwa asilimia mia kuwa wimbo fulani ndio bora. Ndimi za wanadamu huona utamu mbalimbali katika chakula kimoja. Vivyo hivyo masikio na akili.

Hata hivyo wimbo mzuri lazima uwe na lengo fulani la kutimizwa linalokubaliwa katika jamii. Kinachoshangaza siku hizi ni nyimbo za kisiasa. Nyingi hazina hata chembe ya maadili. Lugha si lugha. Baadhi ya video bila kupiga vijembe nina uhakika zilitolewa katika ghala la shetani. Hazitamaniki kamwe. Mtunzi wa nyimbo kama hizi bila shaka nia yake ni kuleta fujo na kuhatarisha amani.

Ni vyema kutunga nyimbo zinazozingatia maadili ya jamii. Hivyo basi serikali na wazalendo wote wapinge nyimbo ambazo hazizingatii maadili na kuleta faida kwa jamii.

6. Je, ni kweli kusema binadamu wote wanakubaliana kwa kauli moja kuwa wimbo fulani ndio bora? **(Ndio au La)** ____________ (al 1)

7. Mwandishi ameuliza maswali mangapi yanayohusiana na muziki katika aya ya kwanza?

____________ (al 1)

8. Kulingana na kifungu hiki, wimbo mzuri ni lazima.

____________ (al 1)

9. Unafikiria ni kwa nini mwandishi amesema video nyingine zilitolewa katika ghala la shetani?

____________ (al 1)

10. Mwisho mwandishi anapendekeza nini kuhusu utunzi wa nyimbo? (al 1)

____________

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la* **11** *hadi la* **13**

Kuwepo kwa tarakilishi kumechangia pakubwa katika kukua kwa uchumi kibiashara na kuboresha, bila kusahau kurahisisha mawasiliano. Kazi zilizofanywa na watu wengi huweza kufanywa kwa kidole kimoja tu.

Zilizochukua siku nyingi zimebaki kufanyika kwa sekunde tu. Hizi ni juhudi za wanasayansi na wahandisi. Miaka imefupishwa na kuwa sekunde, nayo dunia nzima kuwa kitongoji tu. Makabila yakakusanywa pamoja kuwa ni kama mlango mmoja wa ukoo.

Kumbuka uundaji wa tarakilishi ni njia ya mwanadamu kumuiga Mungu. Tarakilishi hufanya kazi nyingi. Zikiwemo kutuma ujumbe, kuhifadhi kumbukumbu, kuendesha mipango mbalimbali na kazi nyingine. Kompyuta pia ni kifaa cha burudani. Kina michezo mbalimbali ya kumstarehesha binadamu. Huweza pia kutumika kuonyesha filamu na kuonyesha muziki.

Tarakilishi imezaa madhara makubwa katika jamii. Hivi leo mfanyikazi mmoja, kwa kutumia kompyuta, anafanya kazi za watu wengi, jambo ambalo limesababisha kuachishwa kazi kwa watu wengi.

11. Taja faida mbili za vile tarakilishi imechangia katika ukuaji wa uchumi. (al 2)
 (i) ____________________
 (ii) ____________________

12. Taja njia mbili za vile tarakilishi imeundwa kuiga Mungu. (al 2)
 (i) ____________________
 (ii) ____________________

13. Taja hasara ambayo imeletwa na kompyuta. (al 1)

____________________

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la* **14** *hadi la* **17**

Usiku huo, kulikuwa na giza totoro. Mvua nayo ilikuwa ikinyesha. Iliandamana na ngurumo za radi. Mbwa wengi walibweka bwebwebwe. Saa mbili baadaye, mvua iliacha kunyesha na upepo ukaanza kuvuma.

Muda baadaye, tulisikia jirani yetu akipiga kelele. Kwanza, tulipuuza kwani jirani alipenda kufanya hivyo kila siku. Tulifikiria alikuwa mlevi.

Kisha baadaye, tulisikia mke na watoto wake nao wakipiga mayowe. Baba alitumia simu yake na kuwaeleza polisi hali ilivyokuwa. Polisi walisema wangefika hapo haraka. Baba alianza kufungua mlango ili aende kwa jirani.

Ghafla bin vu tulisikia mfyatuko wa risasi. Maskini baba alishtuka. Aliangusha simu yake. Baba aliruka na kujificha chini ya meza. Mimi na ndugu yangu tulienda kujificha jikoni.

Dakika chache baadaye, tulisikia king'ora cha gari la polisi. Mapambano makali kati ya wezi na askari yalianza. **Kwa nyota ya jaha**, wezi walishindwa na wakakamatwa. Kweli uhalifu haulipi.

14. Taja mambo yaliyotendeka usiku huo. (al 2)
 (i) ____________________
 (ii) ____________________

15. Kwa nini walipuuza kelele za jirani? (al 1)

____________________

16. Ni nani aliarifu polisi hali ilivyokuwa pale kijijini? ______________ (al 1)

17. 'Kwa nyota ya jaha' ni msemo unaomaanisha ______________ (al 1)

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi* **18** *mpaka* **22**. *Umepewa majibu hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.* **(al 5)**

**18.** ____________ **(Ukataji, Kukata)** miti ovyoovyo kumeliletea taifa matatizo chungu **19.** ____________ **(mzima nzima)**. Mvua **20.** ____________ **(inaendelea, unaendelea)** kupungua nacho kiwango cha joto **21.** ____________ **(kinazidi, inazidi)** kupanda. Mmomonyoko wa udongo umeharibu ukulima wetu **22.** ____________. **(popote, kokote)** tuliko.

*Kutoka swali la* **23** *hadi la* **30**, *jibu sahihi kulingana na maagizo.*

23. Kamilisha methali: Kidole kimoja ______________. (al 1)
**(hakichinji ng'ombe hakivunji chawa)**

24. Baada ya kuongea sana, waliagana bila kujua watakutana lini tena. Mmoja alisema ______________ na mwenzake akamjibu ______________. (al 2)

25. Taja nonimo mbili za pekee. (al 2)
i) ______________
ii) ______________

26. Usafi wa kibinafsi ni muhimu. Taja shughuli mbili za kudumisha usafi wa mwili na mazingira. (al 2)
i) ______________
ii) ______________

27. Taja sifa mbili za fasihi andishi (al 2)
i) ______________
ii) ______________

28. Tunga sentensi mbili zenye sauti (al 2)
i) dh ______________
ii) th ______________

29. Kanusha. (al 2)
i) Ungalimeza dawa maumivu yangalipungua.
______________
ii) Tukiishi kwa amani tutapata maendeleo.
______________

30. Jaza nafasi kwa mnyambuliko wa vitenzi unaofaa. (al 2)

| **Vitenzi** | **Kauli ya kutendeana** | **Kauli ya kutendua** |
|---|---|---|
| **Bandika** | Bandikiana | ______ |
| **Tega** | ______ | Tegua |

JESMA 002

# TATHMINI YA AWAMU AWALIA
## GREDI YA SABA 2024
## - INSHA -

Muda: Dakika 40

Jina la mwanafunzi: .................................................. Nambari ya Tathmini: ....................

Shule: ........................................................................... Gredi 7:................. Tarehe: .......................

**Andika insha ya maelezo kuhusu**

**SIKU YA MICHEZO SHULENI**


© Jesma Publishers & Educational Boosters Ltd. Simu: 0794677748/0701545759